# Mbinu na Mikakati ya Kutumia Fasihi ya Watoto kama Bibliotherapia[1]

Pamela M.Y. Ngugi


## Ikisiri

Katika ulimwengu wa sasa, sanaa ya uchoraji, dansi, muziki na hata fasihi imechukuliwa kama aina moja ya tiba kwa wagonjwa wanaougua magonjwa mbalimbali. Wataalamu wa tiba-therapia wameanza kutumia fasihi kama njia ya kuwasaidia wanajamii kukabiliana na hali mbalimbali za kijamii baada ya kugundua nafasi muhimu ya vitabu katika kutibu wagonjwa na wanajamii wengine wanaopitia hali ngumu za kijamii. Fasihi ya watoto kama ilivyo fasihi ya watu wazima ina majukumu mbalimbali katika jamii yoyote ya binadamu. Kupitia fasihi, wanajamii hujuzwa, huelimishwa na kuburudishwa. Fasihi ya watoto huwa na lengo maalum katika maisha ya watoto kwani inaweza kutumika kama kitulizo cha moyo kutokana na hali mbalimbali zinazowakumba watoto wa kisasa. Hadithi za watoto zinaweza kutumika kama njia mbadala za namna ya kukabiliana na hali ngumu za kimaisha. Usomaji wa vitabu vya fasihi ya watoto unaweza kutumika kama kichocheo cha mijadala ama darasani au hata nyumbani kuhusiana na hali mbalimbali zinazowakumba watoto katika viwango mbalimbali vya ukuaji. Lengo la makala hii ni kubainisha mbinu na mikakati ya kutumia fasihi ya watoto kama bibliotherapia. Katika kutekeleza hili, makala itaeleza dhana ya bibliotherapia pamoja na kubainisha njia mwafaka zinazoweza kutumiwa na wadau hasa walimu katika kutumia vitabu kama bibliotherapia miongoni mwa wanafunzi wao. Pamoja na hayo, mifano ya namna bibliotherapia inavyotumika katika hali mbalimbali za watoto imetolewa.


## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya watoto ni ile iliyoandikwa kwa minajili ya kusomwa na watoto. Hii haimaanishi kuwa fasihi hii haiwezi kusomwa na watu wazima. Fasihi ya watoto huwa imeandikwa kwa kuzingatia msomaji ambaye hasa tajriba yake ya maisha ingali finyu na vilevile uelewa wake wa mambo ungali unakua. Hivyo basi, fasihi hii huwalenga watoto kwa kuwa wao ni binadamu ambao wanaendelea kukua kiakili, kilugha na hata kiumbo (Ngugi, 2012). Taaluma hii inajisimamia ingawa inachukuliwa kuwa na mizizi yake katika fasihi kwa jumla. Fasihi ya watoto, kama sanaa nyingine yoyote, ni chombo chenye misingi yake katika ubunifu. Kwa ujumla ni sanaa inayochochewa na hali halisi katika mazingira ya kijamii. Sanaa hii huweza kueleza matukio ya jamii, ikadhihirisha matumaini na matarajio yao. Kama ilivyo fasihi inayolenga hadhira ya watu wazima, fasihi ya watoto inalenga kuburudisha na kuelimisha (Njogu na Chimerah, 1999).

Kwa muda mrefu, tangu enzi za wanafalsafa kama vile Plato, fasihi imechukuliwa na wanajamii kama chombo cha kuumba fikra za watoto katika jamii. Fasihi huelimisha kwa kupanua mawazo ya watoto kutokana na maisha ya watu wengine. Mtoto anaposoma kazi yoyote ile, huwa anajielewa na kuuelewa ulimwengu anamoishi kupitia matukio katika kazi hiyo. Vilevile, kazi hiyo

[1] Makala hii iliwasilishwa katika Kongamano la RISSEA, 2012, Mombasa, Kenya.

humsaidia kutalii ulimwengu wake, kukuza tajriba na kumpa nguvu za kuweza kukabiliana na hali mbalimbali zinazoweza kumjia. Katika ujumla wake, fasihi hutoa maonyo, mawaidha, makatazo na maelekezo. Hivyo basi, fasihi ya watoto ni njia mwafaka ya kuchuja jamii ya mtoto na kuielekeza. Katika fasihi ya watoto, msanii hujaribu kujenga ulimwengu mzima ambao unafanana na maisha halisi ambayo mtoto anaweza kujinasibisha nao. Katika ulimwengu wa sasa, watoto wamejikuta katika hali tatanishi ambapo wanahitaji ushauri kuhusiana na masuala ibuka katika jamii. Ngugi (2014) anaeleza kuwa watoto bado wanaendelea kukua kimwili, kisaikolojia na wanawategemea watu wazima kuwaelekeza. Mbali na ushauri wa moja kwa moja kutoka kwa wazazi, fasihi inaweza kuchangia katika kumsaidia mtoto kukubali hali fulani na hata kujua namna ya kukabiliana na hali nyinginezo ambazo zitaendelea kuibuka katika maisha yake kila kukicha. Matumizi ya fasihi kama chombo cha kutolea ushauri ndiyo hurejelewa kama bibliotherapia. Lengo la makala hii ni kubainisha namna bibliotherapia inavyoweza kutumika kama njia mbadala ya kuwatuliza watoto wanaopitia katika hali mbalimbali za kimaisha. Katika kulifikia lengo la makala hii, dhana ya bibliotherapia na historia yake imejadiliwa kwa lengo la kuielewa. Pili, tafiti mbalimbali zimehakikiwa ili kuonyesha namna fasihi ya watoto inavyotumika kama chombo cha kutolea nasaha na mwisho kabisa, mapendekezo ya mikakati ya kutumia fasihi kama bibliotherapia miongoni mwa watoto imetolewa.

## 2.0 Dhana na Historia ya Bibliotherapia

Bibliotherapia kama dhana ilianzishwa mwaka 1916 na mtaalamu aitwaye Samuel Crothers (Afolayan, 1992; Pardeck na Pardeck, 1998). Ingawa neno bibliotherapia ndilo linalotumika kwa sasa, zipo dhana nyingine ambazo zinatumika kurejelea dhana hii kama vile ushauri wa kibibliotherapia, bibliotherapia-nafsia, mlinganuo-vitabu, fasihi-matibabu na kadhalika (Pehrsson, 2006). Kimsingi bibliotherapia hurejelea mbinu ya kutumia vitabu ili kuwasaidia watu kupata suluhisho kwa hali mbalimbali zinazowakumba katika kipindi fulani cha maisha yao. Kulingana na Shrodes (1950), bibliotherapia ni harakati ya mwingiliano wenye nguvu kati ya hulka ya msomaji na fasihi chini ya maelekezo ya mtaalamu au mtu aliye na ujuzi fulani.

Matumizi ya usimuliaji wa hadithi na usomaji kama njia ya kutibu ni harakati ambayo imejadiliwa kwa kina katika karne ya 20 ingawa taaluma iliyohusika nayo imebadilika (Pehrsson, 2006). Bibliotherapia ni dhana iliyo na misingi yake katika taaluma ya Sayansi ya Maktaba na imetumiwa hata enzi za Wagiriki ambao walichukulia kuwa fasihi ilikuwa muhimu siyo tu kisaikolojia bali pia kiroho (Sullivan na Strang, 2002). Na kwa sababu hiyo waliweka vibango kwenye maktaba vilivyoeleza maktaba kama mahali pa kuponya moyo. Hoja muhimu katika bibliotherapia ni kwamba usomaji hutoa matibabu ya aina fulani kwa

anayesoma. Inachukuliwa kwamba malighafi za kifasihi huweza kutumiwa kama njia ya kupata suluhisho kwa hali mbalimbali zilizo tata katika maisha ya mwanajamii. Bibliotherapia ilitolewa kwa wingi hasa katika matibabu katika enzi ya baada ya Vita Kuu vya Pili vya Dunia kwa sababu ilibainika kuwa askari wengi waliokuwa wameathirika vitani walikuwa na muda mrefu wa kuweza kusoma huku wakiuguza majeraha yao.

Kwa mujibu wa Sullivan na Strang (2002) bibliotherapia ni harakati ya muingiliano ulio na nguvu kati ya hulka ya msomaji na fasihi. Muingiliano huu huweza kutumika kwa ajili ya kujisaka, kujirekebisha na kujikuza. Dhana ya matibabu haya imeegemea kwa mwelekeo wa binadamu wa kujitambulisha na wengine kupitia kujieleza katika fasihi na sanaa nyinginezo. Kwa sasa, pamebainika tofauti kati ya bibliotherapia aina ya Kliniki ambayo hutekelezwa na mtaalamu wa ushauri au mwanatherapia na bibliotherapia-kuzaji ambayo inaweza kutumiwa na walimu na watu wengine wasio na ujuzi maalum ili kuwaelekeza watoto wanapokua kuhusiana na masuala ya ujitambuaji (Pehrsson, 2006).

## 3.0 Matumizi ya Bibliotherapia kwa Watoto

Kwa mujibu wa Sullivan na Strang (2002), bibliotherapia inahusu mtoto kusoma kitabu kilicho na mhusika ambaye ameweza kukabiliana na hali fulani na kuishinda. Hali kama hii inahitaji kuwa sawa na ile ambayo mtoto huyu anayesoma anaipitia. Kauli hii inatokana na ukweli kwamba kitabu kinaweza kumzungumzia mtoto kwa njia nzuri kabisa kuliko ambavyo mtu mzima angekuwa anatekeleza jukumu hilo (Maich na Kean, 2004). Bibliotherapia inaweza kuwasaidia watoto kukabiliana na hali mbalimbali katika maisha. Vitabu humfichulia mtoto hali halisi za maisha ambazo huenda zikawa tofauti na tajiriba anazopitia mtoto huyo. Ujitambulishaji wa mhusika kielelezo wa kifasihi unaweza kukuza mawazo ya kufikiria namna ya kujitoa katika hali fulani kama vile kukubali utengano na talaka kwa wazazi, magonjwa, kifo, umaskini, ulemavu, ukengeushi, maafa, vita na mengine mengi.

Parker (2005) anaona kuwa bibliotherapia imetumika kwa muda mrefu kwa wanafunzi walio na matatizo ya kujifunza na ya kitabia. Watoto kama hawa huhisi kuwa wamekataliwa na marika, hawana mbinu za mahusiano ya kijamii na hawajiamini. Wanafunzi wote wanaweza kufaidika kutokana na mbinu hii maana kila mwanafunzi hupitia hali hii kwa njia moja au nyingine. Kwa mujibu wa Kavanaugh na Fiorini (2009) msingi wa bibliotherapia ni kwamba ufasiri wa hadithi ni harakati inayobadilika kila wakati na ambayo watoto huleta mahitaji na tajriba zao. Kwa kuwa watoto wengi hupata ugumu kutambua wazi na hata kueleza hisia zao kuhusiana na hali wanazoziptia, hadithi huweza kutumika kama kisaidizi cha majadiliano na ujitambulishaji. Watoto wakihusishwa zaidi na wahusika wa kifasihi, wanaweza kutoa kauli zao, au wakaigiza wahusika na hata kujieleza

kupitia uchoraji wa picha katika kueleza fikra zao za ndani. Kwa mujibu wa Kavanaugh na Fiorini (2009), katika hali kama hii fasihi inatumika kama sauti ya watoto ambao hawawezi kujieleza na hata kuendeleza ujitambulishaji zaidi na kujikubali hasa kwa watoto wanaojikuta kuwa wametwaliwa. Kupitia kusoma namna watoto wengine walivyokabiliana na hali hiyo au kule kupewa mtazamo mwingine, watoto hawa wanaweza kutambua na kubuni mbinu zilizo faafu za kukabiliana na hali hiyo ya kuwa na wazazi-walezi. Vilevile, katika kurejelea watoto waliotwaliwa, mkabala wa kibibliotherapia unaweza kutumiwa na wazazi-walezi waliowatwaa watoto hao kuwahalalishia hisia zao kuhusu hali hiyo, na kuwahakikishia kwamba ni vyema kwao kuizungumzia hali hiyo ya kutwaaliwa. Katika kufanya hivi watakuwa wakisimika uhusiano wao ambao utawasaidia watoto kukua kifikra na hata kuweza kupona kihisia. Kwa ujumla ni kwamba bibliotherapia inaweza kutumiwa kama chombo cha kutoa tahadhari, na kumtayarisha mtoto kwa hali ambazo zinaweza kutokea katika maisha yake ya baadaye.

**4.0 Malengo ya Bibliotherapia**

Matumizi ya bibliotherapia hulenga katika kutimiza malengo yafuatayo:

- kutambua na kuthibitisha hisia za mtoto-msomaji;
- kumwezesha mtoto-msomaji kutambua kuwa watoto wengine hupitia hali kama hizo anazopitia;
- kuzindua mijadala;
- kuendeleza fikra na kujifikiria mwenyewe;
- kutambua mbinu bora za kustahimili na kupata suluhu; na
- kuamua hatua ya kuchukua baadaye.

**5.0 Mbinu za Kutumia Fasihi ya Watoto kama Bibliotherapia**

Kwa mujibu wa Prater, Johnstun na Munk (2005) na Parker (2005) walimu pamoja na wadau wengine wanaweza kuwasaidia watoto kutumia bibliotherapia kupitia viwango vitatu ambavyo ni: utambulisho, utakaso-hisia na umaizi. Utambulisho unadhihirika pale msomaji anapojitambulisha na wahusika au hali fulani katika kazi ya fasihi. Utambulisho huu hutokana na kuelewa na kuona jinsi kazi fulani inavyoakisi uhalisi na kutoa kauli kuyahusu maisha na watu wenyewe na jinsi inavyochochea msomaji kuijenga maana fulani kwa kuyafungamanisha maisha yao na taswira fulani. Utakaso-hisia unatokea pale msomaji anaposhiriki katika fikra na hisia za mhusika, na umaizi hubainika pale msomaji anapotambua kwamba anahusiana na mhusika au hali fulani na anajifunza namna ya kukabiliana vilivyo na hali tata za maisha hayo. Cleveland (2008) anaongeza kiwango cha nne ambacho ni cha ubia. Hiki ni kiwango ambacho mtoto huweza kutambua kuwa binadamu ulimwenguni kote hupitia katika hali mbalimbali za kimaisha. Kwa

hivyo, bibliotherapia ni chombo muhimu cha kuanzisha mawasiliano kati ya mtu mzima na mtoto kuhusu hali wanazopitia. Ufaafu wa bibliotherapia ni kwamba inawapa watoto nafasi ya kuwa na mtazamo wa utonafsi (*objective*) katika kuchunguza hali zao wenyewe na kujaribisha hisia zao na miitikio yao katika mazingira yasiyohatarisha (Kavanaugh na Fiorini, 2009).

## 6.0 Hatua za Utekelezaji wa Bibliotherapia

Pardech (1993) akimnukuu Scrodes (1950) anapendekeza hatua tatu za utekelezaji wa bibliotherapia. Hatua hizo ni:

- ubainishaji wa mahitaji yake;
- uteuzi wa kitabu ambacho kinalandana na mahitaji ya mtoto; na
- Uwasilishaji wa hadithi kwa Watoto.

Kimsingi kielelezo hiki hutumika katika hadithi za kubuni kuliko katika fasihi-arifa. Ufafanuzi wa hatua hizi zinatolewa katika sehemu ifuatayo.

## 6.1 Ubainishaji wa Mahitaji ya Watoto

Wanasaikolojia wengi wanakubaliana kuwa kuelewa mahitaji ya kimsingi ya watoto ni hatua muhimu katika kufanikisha masomo yao. Kwa mfano, Salehi (2011) anaeleza kuwa watoto wote huwa na mahitaji ya kisaikolojia; na kwamba hisia za watoto huwa dhaifu kiasi kwamba mahitaji haya yakipuuzwa basi watoto wataweza kukabiliana na matatizo mengi katika siku za mbeleni. Hivyo basi, ili kupata mafanikio katika maisha ya watoto ya baadaye, ni muhimu kutambua mahitaji yao ya kimsingi, pawe na jitahada za kusuluhisha matatizo fulani wanayokumbana nayo na suluhu zinazotolewa zinahitaji kuwa zenye mantiki na zilizosawazishwa. Watoto huwa na mahitaji tofauti na wao hudhihirisha kuwa wanawategemea wazazi kuwatekelezea mahitaji haya. Mahitaji ya msingi kwa watoto ni: lishe bora, kutaka kuzingatiwa na kuishi katika hali ya usalama. Mbali na mahitaji haya ya kimwili, watoto pia huhitaji kudadisi na kutekeleza udadisi huo. Wao hutaka kudadisi mazingira yao kiuhalisi na kisaikolojia. Kwa sababu hiyo ni muhimu kufikiria kuhusu mada zinazofaa kwa kila mtoto katika vitabu vya watoto na vijana. Jambo hili litachangia katika kutimiza hamu yao ya udadisi. Ngugi (2014) anaeleza kuwa, ili mtoto aweze kufaidika kutokana na kile anachokisoma, ujumbe wa hadithi husika unahitaji kumhusu mtoto huyo. Katika kufanya hivi, mtoto huyu atakuwa anasoma kile ambacho kinaweza kumsaidia katika maisha yake, kwa mfano,inaweza kuwa kudhibiti hisia mbalimbali, kubadilisha mwenendo fulani au hata kupata maarifa kuhusiana na jambo fulani.

### 6.2 Uteuzi wa Vitabu

Uteuzi wa kitabu faafu hauna budi kufanywa kwa mujibu wa mtazamo wa mtoto. Mambo kama vile umri, ukomavu wa kiakili, kiwango cha elimu, shauku na tatizo linalohusika huhitaji kuzingatiwa kwa makini zaidi. Ikiwa mtoto atashindwa kujitambulisha na wahusika katika hadithi au apoteze hamu ya kukisoma kitabu hicho, basi hataweza kung'amua maana ya hadithi hiyo na mwishowe kitabu kitakosa kufikia malengo ya kutoa utakaso-hisia na hata matibabu yaliyodhamiriwa (Kavanaugh na Fiorini, 2009).

Kwa ujumla, vipo vigezo vya kimsingi ambavyo hutumika katika kuwateulia watoto vitabu vya kusoma. Kwa mujibu wa wakuza mitaala nchini Kenya (Ministry of Education, 2002) vigezo hivi ni pamoja na:

- mtindo sahili unaofaa katika utunzi wa vitabu vya watoto;
- lugha inapaswa kuafiki kiwango cha utambuzi wa mtoto;
- msamiati usiwe mgumu kiasi cha kumwelemea mtoto anaposoma;
- msamiati uambatane na mazingira ambamo mtoto anaweza kufahamu; na
- wahusika wakuu wanapaswa kuwa watoto na sharti wasawiriwe kwa njia ya kuaminika.

Mbali na vigezo hivi, wataalamu wengine ambao wameshughulikia bibliotherapia kama vile Parker (2005), Cleveland (2008) na Kavanaugh na Fiorini (2009) miongoni mwa wengine, wanapendekeza sifa zifuatazo zizingatiwe:

- kitabu kilichoteuliwa kinahitaji kuwa na hadithi inayovutia;
- tatizo linaloshughulikiwa pamoja na suluhisho linahitaji kuaminika na wala lisitoe matumaini yasiyo kweli;
- mhusika mkuu anahitaji kuwa kielelezo bora, anayedhihirisha mbinu faafu za kukabiliana na hali hiyo;
- pasiwe na mambo fulani katika kitabu hicho ambayo yatamfadhaisha, kumchanganya na hata kumwumiza zaidi mtoto msomaji;
- mtoto aweze kujitambulisha na mhusika mkuu;
- hadithi husika imtulize mtoto;
- hadithi hiyo ilenge umri wa mtoto;
- kitabu kiwe na picha za kuvutia;
- watoto wengine wanapoisoma hadithi waweze kuwa wepesi wa kuhisi hali mbalimbali wanazopitia wenzao; na
- hadithi iwe na uwezo wa kupokelewa na tamaduni mbalimbali.

### 6.3 Uwasilishaji wa Hadithi kwa Watoto

Ili kuhakikisha kuwa kazi fulani ya fasihi itamsaidia mtoto, zipo mbinu kadha wa kadha ambazo zimependekezwa na wataalamu wa fasihi ya watoto katika

kuwatanguliza kwa usomaji na hata kunasa na kuendeleza umakini wa usomaji wa hadithi fulani. Mbinu hizi zinaweza kutumika katika bibliotherapia. Mbinu zifuatazo zimependekezwa na Potyaeva (2005) na Ngugi (2011):

**Jedwali 1: Mbinu za Uwasilishaji wa hadithi kwa Watoto**

| Kabla ya Usomaji | Wakati wa Kusoma | Baada ya Kusoma |
|---|---|---|
| • Utoaji wa maoni<br>• Ujengaji wa matarajio<br>• Ubashiri wa mwisho wa hadithi<br>• Uonyeshaji vielezo<br>• Utoaji mifano<br>• Kufikiria kwa sauti<br>• Kuuliza maswali na kujadili<br>• Kuteua kitabu cha kusoma<br>• Usomaji wa kujitegemea | • Kusoma kwa sauti<br>• Kutunga nyimbo kutokana na hadithi<br>• Kuelekeza katika usomaji<br>• Kutenga wakati wa kutulia na kufikiria<br>• Kusoma-kutulia - kujadili<br>• Kutalii kila sura ya hadithi<br>• Kujitathmini<br>• Kuwaza na kujenga taswira<br>• Kusikiliza na kusoma<br>• Usomaji kimakundi | • Mbinu za ufahamu<br>• Kutoa mahitimisho<br>• Kurejelea makala mengine na hata kuwa na ufahamu wa awali wa mambo (tajriba za awali)<br>• Kujifunza mbinu za mpangilio wa makala<br>• Kuhusisha taswira ya fasihi na hali halisi ya maisha |

## 7.0 Nafasi ya Walimu katika Kuendeleza Bibliotherapia

Katika enzi hizi za utandawazi, elimu imeanza kuchukua mwelekeo wa kuingiliana kwa taaluma mbalimbali, mwelekeo ambao unawahitaji walimu kushirikiana na idadi kubwa ya watu kutoka taaluma nyinginezo (Maich na Kean, 2004). Ushirikiano wa aina hii ni mbinu mwafaka inayotumiwa na wataalamu mbalimbali ambao hutoa huduma kwa watoto katika enzi hizi za ujumuishaji. Katika shule nyingi, kuna watoto kutoka misingi mbalimbali ya kijamii hali ambayo inaweza kuleta kutoelewana miongoni mwa watoto wenyewe na hata walimu. Kutokana na hali hii, walimu wanajikuta wanatekeleza, kwa njia moja au nyingine, majukumu yanayopaswa kutekelezwa na wataalamu wengine. Kwa mfano, Maich na Kean (2004) wakimnukuu Hayes (1995) wanaeleza kuwa taaluma ya Saikolojia inaweza na inahitaji kutumiwa na hata wale wasio wanasaikolojia. Pia, wanaona kuwa shule ni mazingira muhimu ya kutumiwa elimu hii. Ukweli ni kwamba walimu wengi wawapo darasani hujikuta wakitekeleza majukumu ya wanasaikolojia au wakifanya kazi ya wanatherapia kwa njia iliyo rasmi au isiyo rasmi. Jukumu hili linaweza kuchukuliwa kuwa ni uendelezaji wa ukuaji na mabadiliko kwa mteja. Katika shule na madarasa yanayojumuisha wanafunzi kutoka misingi mbalimbali ya kijamii, walimu hujikuta wanashughulikia mahitaji mbalimbali ya wanafunzi kwa sababu kila mwanafunzi huwa anapitia tajriba mbalimbali za kijamii na kihisia katika maisha yake. Hivyo basi, wanafunzi wote wanaweza kufaidika kutokana na ujifunzaji wa mbinu mwafaka za kukabiliana na changamoto

mbalimbali wanazokumbana nazo shuleni na hata nyumbani. Katika hali kama hizi walimu wanaweza kutumia mbinu ya bibliotherapia katika kuwaelekeza wanafunzi wao mbinu mwafaka za kukabiliana na hali zao. Ili kulifikia lengo hili, Maich na Kean (2004) wanasema kuwa mwalimu atahitaji kuzingatia mambo yafuatayo:

- mazingira faafu;
- tatizo la kushughulikia lililo wazi;
- marejeleo yaliyo na maelezo ya kina; na
- mpangilio maalum wa masomo.

Waitifaki wa bibliotherapia (taz. Carlson, 2001) wamependekeza kuwa ili pawe na mafanikio katika utekelezaji wa mbinu hii pana umuhimu wa kuwapo kwa mazingira yanayofaa. Mazingira haya yatajumuisha hali zifuatazo:

- utulivu na heshima;
- uaminifu na mapatano; na
- uelewa wa watoto, fasihi, usomaji na lugha.

## 8.0 Changamoto katika Kupata Hadithi Zinazofaa

Kazi ya kupata hadithi inayofaa ya kutumia kama bibliotherapia inaweza kuwa changamaoto kubwa kwa mwalimu hasa anayefunza nchini Kenya. Hii inatokana na sababu kuwa hakuna bibliografia iliyo na maelezo ya kina (*annotated bibliography*) kuhusu fasihi ya watoto iliyochapishwa kwa kazi hii. Kwa mfano, kitabu cha *Approved List of Primary and Secondary School Textbooks and other Instructional Materials* maarufu kama “Orange Book” ambacho huchapishwa kila mwaka na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala kimetoa tu orodha ya vitabu vya fasihi ya watoto wa viwango mbalimbali wala sio maelezo ya vitabu hivi. Katika hali kama hii mwalimu hujikuta katika msitu wa vitabu bila kujua yaliyomo katika vitabu hivyo na matokeo yake anaweza kushindwa kutekeleza kazi yake vilivyo. Hata hivyo, hali hii inaweza kusuluhishwa iwapo walimu wataongozwa na wakutubi wa shule katika kuviteua na kupanga vitabu kulingana na mada ambazo mwalimu angependa wanafunzi wake wazisome. Jambo jingine kwa mwalimu ni kuzingatia vigezo vya kuteua fasihi nzuri kwani hadithi hizo zinahitaji kudhihirisha usanii licha ya kuwa na mafunzo mazuri.

## 9.0 Mifano ya Matumizi ya Bibliotherapia

Udurusu wa vitabu unaonyesha kwamba mbinu ya bibliotherapia imepata msingi imara katika miaka ya 1990 (Pehrsson na Mcmillen, 2005) na imetumiwa na wataalamu mbalimbali na kwa viwango mbalimbali vya watu. Miongoni mwa waliotumia mbinu hii ni pamoja na washauri wa shule, wafanyakazi wa jamii, wauguzi wa magonjwa ya kiakili, walimu na wakutubi. Mbali na hayo, zimo hali

mbalimbali ambapo bibliotherapia imetumiwa na watu mbalimbali. Kwa mujibu wa Pehrsson na Mcmillen (2008), hali zifuatazo zimetumiwa na wataalamu waliotajwa: udhalimu (Shechtman, 1999, 2000), kutwaaliwa kwa mtoto / kupanga mtoto (Pardeck, 1993; Sharkey, 1998), utambuzi wa tofauti miongoni mwa watu (Pardeck na Pardeck, 1998; Tway, 1989), kifo/kuugua (Meyer, 1994; Todahl, Smith, Barnes na Pereira, 1998), matumizi ya madawa ya kulevya (Pardeck, 1991), talaka (Early, 1993; Kramer na Smith, 1998; Meyer, 1991), udhihirishaji wa talanta maalum (Hebert, 1995), usuluhishwaji wa migogoro (Hodges, 1995), utesaji wa watoto/ kutowatunza watoto (Jasmine-De Vias, 1995; Pardeck, 1990), jinamizi (Barclay na Whittington, 1992), mfadhaiko (Ackerson, Scogin, McKendree-Smith na Lyman, 1998), kuachana na kumpoteza mwanajamii (Bernstein na Rudman, 1989), watoto wanaoteswa katika familia (Butterworth na Fulmer, 1991), wingitamaduni (Pardeck na Pardeck, 1998) na ukosefu wa makao (Farkas na Yorker, 1993). Kama orodha hii inavyoonesha mbinu hii imetumika zaidi na imefanyiwa utafiti mwingi katika mataifa mengine ya Marekani na Ulaya kuliko ilivyo nchini Kenya na hata nchi nyingine za bara la Afrika. Upo uwezekano wa kupendekeza mbinu hii itumike katika shule za Kenya na nchi zingine katika bara la Afrika. Hii ni kutoka na sababu kuwa mbinu za kukabiliana na hali fulani zinaweza kuendelezwa miongoni mwa watoto. Katika kufanya hivyo, hisia hasi kama vile dhiki, dukuduku na upweke huweza kupunguzwa na badala yake mtoto akaweza kujipa taadhima na mbinu faafu za mahusiano ya kijamii kuendelezwa pamoja na kupata hisia komavu (Afolaya, 1992).

## 10.0 Hitimisho

Ili kuwapo na mafanikio katika kuwaelimisha watoto kwa njia ambazo zitawasaidia sasa na baadaye, umuhimu wa elimu usitegemezwe tu kwa masuala ya kiakademia ya watoto pekee yake bali ifahamike kuwa masuala ya kijamii na kihisia yanahitaji kujumuishwa ili kumkuza mtoto kama binadamu aliyekamilika. Bibliotherapia inaweza kumkuza mtoto katika ukamilifu na ukomavu wa kuweza kukabiliana na changamaoto za maisha za sasa na baadaye. Ufanisi wa bibliotherapia utabainika iwapo mtoto ataweza kujitambulisha kwa kutumia hadithi aliyoisoma. Vile vile, tunaweza kujua iwapo mtoto amefaidika na mbinu hii iwapo tunaweza kuona mabadiliko ya kihisia na hata kitabia au iwapo mtoto ameweza kukabiliana hali fulani ya kijamii kwa uthabiti. Ili kufanikisha harakati hii panahitajika mazingira tulivu na heshima, uaminifu na mapatano kati ya msomaji na wadau pamoja na uwezo wa watoto kuelewa hadithi wanazopewa.

## Marejeleo

Ackerson, J., Scogin, F., McKendree-Smith, N., & Lyman, R. D. (1998). "Cognitive Bibliotherapy for mild and moderate adolescent depressive symptomatology". In: *Journal of Consulting & Clinical Psychology,* 66(4), 685-690.

Afolayan, J.A. (1992). Documentary Perspective of Bibliotherapy in Education. In: *Reading-Horizons,* 33(2), 137-148.

Barclay, K. H., & Whittington, P. (1992). "Night scares: A literature-based approach for helping young children". In: *Childhood-Education*, 68(3), 149-154.

Bernstein, J. E., & Rudman, M. K. (1989). *Books to help children cope with separation and loss: An annotated bibliography.* Volume 3. New York: R.R. Bowker.

Butterworth, M. D., & Fulmer, K. A. (1991). The effect of family violence on children: Intervention strategies including Bibliotherapy. *Australian Journal of Marriage & Family*.

Carlson, R. (2001). Therapeutic use of story in therapy with children [Electronic version].In: *Guidance & Counseling*, 16(3), 92-99.

Cleveland, A. (2008). "Bibliotherapy for all: Using Children's Literature about Loss and Grieving to increase awareness, develop coping skills, and build Community among Elementary School Student". Webster University.

Early, B. P. (1993). "The Healing Magic of Myth: Allegorical tales and the treatment of children of divorce. In: *Child & Adolescent Social Work Journal*, 10(2), 97-106.

Farkas, G. S., & Yorker, B. (1993). "Case studies of Bibliotherapy with homeless children." In: *Issues in Mental Health Nursing*, 14(4), 337-347.

Hebert, T. P. (1995). "Using biography to counsel gifted young men". *In: Journal of Secondary Gifted Education*, 6(3), 208-219.

Hodges, J. (1995). "Conflict resolution for the young child". In: ERIC Document Reproduction Service ED 394 624.

Jasmine-DeVias, A. (1995). "Bibliotherapy: Books that can play a role in helping children work through some of the effects of abuse and neglect". In: *New England Reading Association Journal*, 31(3), 2-17.

Kavanaugh, C. A., & Fiorini, J. J. (2009). *Uses of Bibliotherapy for adoptive children and their families.* Makala iliyowasilishwa katika Kongamano la *The American Counseling Association Annual Conference and Exposition, Charlotte, NC.*

Kramer, P. A., & Smith, G. G. (1998). "Easing the pain of divorce through children's literature". In: *Early Childhood Education Journal*, 26(2), 89-94.

Lehr, F. (1981). "Bibliotherapy". In: *Journal of Reading*. 25 (1), 76-79.

Maich, K. and Kean, S. (2004). "Read two books and write me in the Morning" Bibliotherapy for Social Emotional Intervention in the inclusive Classroom". In: *Teaching Exceptional Children Plus*. Vol. 1, Issue 2, Article 5. Http://escholarship.bc.ed/education/tecplus/vol1/iss2/5 20-8-2012.

Meyer, M. J. (1991). "Split decision: A Bibliotherapy guide for children who are experiencing divorce". In: *Lutheran Education*, 126, 252-266.

Meyer, M. J. (1994). "Mortal thoughts: A Bibliotherapeutic guide to books for children about death and dying". In: *Lutheran Education*, 129(1), 211-223.

Ministry of Education (2002). *Approved List of Primary and Secondary School Textbooks and other Instructional Materials.* Nairobi: Ministry of Education.

Njogu, K. & R. Chimerah (1999). *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ngugi, P. M.Y. (2011). "Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika shule za Msingi Nchini Kenya"

Katika: P.S. Malangwa na L.H. Bakize (wah) *Kioo cha Lugha* Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Chuo cha Dar es Salaam: TATAKI. 84-94.

Ngugi, P.M.Y. (2012). "Mitaala ya Kiswahili Katika Elimu na Utaifa: Nafasi ya Fasihi ya

Watoto katika Uendelezaji na Uimarishaji wa Utaifa". Katika: Momanyi, C. na wengine (Wah.), *Kiswahili na Utaifa Nchini Kenya.* Nairobi: Twaweza Communications. 90 -104.

Ngugi, P. M.Y. (2014). "Fasihi ya Watoto katika kutekeleza Mahitaji ya Mtoto Kisaikolojia." Katika: D.P.B. Massamba na L.H. Bakize (wah) *Kiswahili.* Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Chuo cha Dar es Salaam: TATAKI. 170 -180.

Pardeck, J. T. (1990). "Bibliotherapy with abused children". In: *Families in Society*, 71(4), 229-235.

Pardeck, J. T. (1991). "Using books to prevent and treat adolescent chemical dependency". In: *Adolescence*, 26(101), 201-208.

Pardeck, J. T. (1993). "Literature and adoptive children with disabilities". In: *Early Child Development and Care*, 91, 33-39.

Pardeck, J. T., & Pardeck, J. A. (1998). "An exploration of the uses of children's books as an approach for enhancing cultural diversity". *Early Child Development & Care*, 147, 25-31.

Parker, K. L., (2005) "Reading for Character: Principles of Bibliotherapy Applied to Children's Literature." *Faculty Publications and Presentations.* Paper 2. http://digitalcommons.liberty.edu/educ_fac_pubs/2 9- 8-2016.

Pehrsson, D. E. (2006). "Benefits of Utilizing Bibliotherapy within play therapy." In: *Play Therapy*, 1 (2), 10-14.

Pehrsson, D. E. & McMillen, P. S. (2008). A Bibliotherapy Evaluation Tool: Grounding

Counselors in the therapeutic use of literature. http://digitalscholarship.unlv.edu/lib_articles/31/ 12-8-2016.

Potyaeva, T. (2005). "On the way to Changing the Future". Katika Gerry Shiel (mhr) *Proceedings of the 14th European Conference on Reading. Zagreb, Croatia. Croatian Reading Association*. 345-347.

Prater, M.A., Johnstun, M., & Munk, J.A. (2005). From Spaceman to the Added Touch: Using

Juvenile literature to teach about Attention Deficit Hyperactivity Disorder. *Teaching Exceptional Children. Plus,* 1(4) Article 4. Tarehe 10-8-2016 http://escholarship.bc.edu/education/tecplus/vol1/iss4/4

Salehi, A. (2011). "Foundations and Principles of Psychological Content of Children's Books." Karatasi iliyowasilishwa katika Kongamano la Fasihi ya watoto. Bangkok. Psrcentre.org./ images/extraimages/36pdf. 9-8-2016.

Sharkey, P. B. (1998). "Being adopted: Books to help children understand--Update 3". In: *Emergency Librarian*, 25(4), 8-10.

Shechtman, Z. (1999). "Bibliotherapy: An indirect approach to treatment of childhood aggression." *Child Psychiatry & Human Development*, 30(1), 39-53.

Shechtman, Z. (2000). "An innovative intervention for treatment of child and adolescent aggression: An outcome study". *Psychology in the Schools*, 37(2), 157-167.

Shrodes, C. (1950). Bibliotherapy: A theoretical and clinical-experimental study (Doctoral dissertation, University of California, Berkeley, 1950). Dissertation Abstracts Online.

Sullivan, H.K. & Strang, H.R. (2002). "Bibliotherapy in Classroom: Using Literature to promote
the development of emotional Intelligence" In: *Childhood Education*. 79 (2), 74 -80.

Todahl, J. Smith, T.E., Barnes, M., & Pereira, M. G.A. (1998). "Bibliotherapy and perceptions of death by young children." *Journal of Poetry Therapy*, 12(2), 95-107.

Tway, E. (1989). "Dimensions of multicultural literature for children". In: M. K. Rudman (Ed.), *Children's literature: resource for the classroom*). Norwood, MA: Christopher-Gordon Publishers, Inc. 109-132.